BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Tisa – Tarehe 21 Mei, 2018.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

142. MHESHIMIWA SIMAI MOH'D SAID (Jimbo la Tunguu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Kwa kuwa Muungano wetu ni Umoja wetu kama waasisi wetu Mwalimu Nyerere pamoja na Mzee Karume walivyotuachia Jamhuri yetu. Hata hivyo, hivi karibuni kumekuwa kunatolewa lugha za kuutia ufa Muungano wetu ambapo baadhi ya Wabunge kutoka Tanzania Bara na Wana CCM wamekuwa wakiongea lugha za kuikejeli Zanzibar na wananchi wake.

(a) Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya mazungumzo na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano ili kuhakikisha hatua za kinidhamu zinachukuliwa bila kuingilia mamlaka ya Bunge.

(b) Je, ni kwa nini Serikali haitoi tamko na inakuwa kimya pale ambapo Mbunge anaongelea lugha zisizo sahihi na kuleta ufa kwenye Muungano wetu.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

122. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Hapa mjini, eneo la Mwanakwerekwe lililotengwa kwa ajili ya kuzikiwa linaonekana kujaa kutokana na kuzikwa watu kila siku. Hadi sasa hakuna eneo jengine lililotengwa kwa ajili hiyo pamoja na kuwa kuna maeneo mengine ya jadi ambayo watu wanazikana.

(a) Je, suala la kutengwa kila Jimbo kukawa na maeneo ya kuzikana kwa wageni na wenyeji wasiokuwa na maeneo yao ya kuzikana.

(b) Je, kama yapo maeneo hayo tayari yamepangwa kwa kutengwa rasmi ili kutoa hofu kwa wageni.

(c) Je, ni maeneo yepi yaliyotengwa kila Jimbo ya kuzikana kwa watu wasio na maeneo ya kuzikana.

Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

85. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

Kwa kuwa msimu wa 2017/2018, watalii wengi walitembelea nchi yetu jambo ambalo limechangia kwa kiasi kikubwa kuongeza mapato. Na kwa kuwa Wizara imejipanga vizuri kuutangaza utalii wetu nchi za nje ili watalii wajionee vivutio vingi vikiwemo vivutio vilivyopo Pemba.

(a) Je, kwa msimu huu hadi kufikia mwezi wa Februari 2018, ni watalii wangapi waliotembelea Zanzibar moja kwa moja kutoka kwao.

(b) Je, ni watalii wangapi waliotembelea Zanzibar wakianzia Tanzania Bara.

(c) Wizara ina mkakati gani wa kuhakikisha watalii wanaoingia hapa Zanzibar wanapata fursa ya

kuvitembelea visiwa vyetu vyote Unguja na Pemba ili kujionea vivutio vilivyopo kwenye visiwa hivi.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

111. MHESHIMIWA HIDAYA ALI MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Miezi michache iliyopita, Wizara imefanya utaratibu wa kuyapima maeneo ya Kizimbani hali iliyoleta wasiwasi kwa wananchi wa maeneo hayo kuwa huenda wakahamishwa wakati wameshakuwepo katika maeneo hayo vizazi kadhaa na hawana pengine pakwenda. Ingawa kumekuwa na maelezo kuwa utaratibu huo ni wa kawaida.

(a) Je, nini makusudi ya Serikali kuyapima maeneo hayo.

(b) Je, Serikali inatoa tamko gani kwa wananchi wa Kizimbani ambao wanaishi kwa hofu ya kuhamishwa maeneo hayo.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

12. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Muyuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Hivi karibuni Serikali imepokea idadi ya walimu wapatao 16 kutoka nchini Nigeria kwa ajili ya kuziba pengo la uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi.

(a) Je, mgawanyo wa walimu hao kwa skuli za Unguja na Pemba ukoje.

(b) Idadi hiyo ya walimu inatosheleza.

(c) Je, mahitaji halisi ya walimu kama hao yakoje.

Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

29. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Kumekuwa na malalamiko ya wananchi waliyoyashika mashamba ya eka tatu hasa Kisiwani Pemba kwamba muda waliopewa kuyahudumia mashamba hayo umekuwa mkubwa ambapo baadhi yao wameshayahudumia mashamba hayo kwa takriban miaka 20 sasa. Pamoja na kupeleka maombi kunakohusika muda mrefu ili wapewe mashamba hayo kisheria.

(a) Je, Waziri jambo hili unalifahamu.

(b) Je, ni lini suala hili litapatiwa ufumbuzi.

Wizara ya Afya:

48. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa Serikali ilitenga jumla ya Tshs. bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za madaktari katika hospitali ya Abdalla Mzee ambazo zitajengwa ndani ya eneo la hospitali hiyo kwa lengo la kuondokana na kukodi nyumba kwa bei kubwa na kupunguza tatizo la madaktari kukaa maeneo ya mbali na hospitali hiyo.

(a) Je, hadi sasa mpango wa ujenzi wa nyumba hizo umefikia hatua gani.

(b) Je, kuna hatua gani za makusudi zilizochukuliwa na Wizara za kuwapatia madaktari wa hospitali ya Abdalla Mzee nyumba za kuishi ili kuhakikisha kwamba wanakaa maeneo ya karibu na hospitali ili kuwapunguzia kero la kusafiri na kuweza kutoa huduma muafaka na kwa wakati.

II. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka 2018/2019.

Zanzibar,
21 Mei, 2018.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.